**Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (United Nations Convention to Combat Desertfication – UNCCD)**

## 1. Utangulizi

Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*United Nations Convention to Combat Desertification – UNCCD*). Mkataba huu ni kati ya Mikataba mitatu iliyopitishwa kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira na Maendeleo (*United Nations Conference on Environment and Development - UNCED*) uliofanyika Jijini Rio De janeiro nchini Brazil mwaka 1992. Mkataba ulitiwa saini Aprili 1994 Paris, Ufaransa na ulianza kazi 26/12/1996. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 19 Juni, 1997 na mpaka sasa Mkataba huu unajumla ya nchi wanachama mia moja tisini na saba (197) Duniani kote. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, inaratibu na kusimamia shughuli chini ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na Miradi inayolenga utekelezaji wa shughuli za Mkataba hasa Matumizi bora na endelevu ya ardhi (*Sustainable Land Management – SLM*), kushiriki mikutano ya nchi wanachama (*Conference of Parties – COPs*); Mikutano ya kupitia utekelezaji wa Mkataba (*Conference to review implementation of the Convention – CRIC*); Mikutano ya Kamati za Kisayansi za Mkataba (*Committee for Science and Technology – CST*) mafunzo mbalimbali.

## 2. Lengo la Mkataba

Lengo la mkataba ni kama ifuatavyo:

Mkataba wa UNCCD unalenga kuzijengea uwezo nchi zilizoathirika na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame ili ziweze kupunguza madhara yatokanayo na hali hii.

Ili kufikia lengo hili, kifungu cha 9 (1) (Article 9 (1), kinazitaka nchi wanachama kuandaa Programu za Kitaifa za kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame kwa njia shirikishi na kuanzia ngazi ya msingi (*National Action Programmes to combat desertification - NAPs*). Lengo la NAP ni kuainisha visababishi vya kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na kubuni njia muafaka za kupambana na visababishi hivyo na madhara yake hususan ukame.

Mipangokazi katika ngazi ya kanda ndogo na kanda zinaainisha changamoto mbalimbali zinazoweza kushughulikiwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya nchi za kanda ndogo. Sambamba na kuandaliwa kwa NAP, Sekretarieti ya Mkataba ilizitaka pia nchi wanachama kuandaa Shabaha za Kuondoa uharibifu wa Ardhi (Land Degradation Neitrality Targets – LDN); kuandaa Mpango kazi wa kutekeleza Jitihada za Ukuta wa Kijani chini ya chni ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) (Great Green Wall Initiative – GGWI Action

Plan) na Mpango wa Kitaifa wa kudhibiti Ukame (National Drought Plan). Nyaraka zote hizi zimekamilika na mpanbo wa utekelezaji upo katika maandalizi.

3. **Ushiriki wa mikutano**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishiriki Mikutano chini ya Mkataba huu tangu kuanzishwa mnamo mwaka 1992. Pia, Nchi wanachama zimekuwa zikiandaa taarifa ya utekelezaji wa Shughuli chini ya Mkataba kila baada ya miaka minne. Taafifa hii huandaliwa kwa njia maalum ya mtandao inayoitwa Performance Review and Assassment of Implamentation System – PRAIS.

4. **Majukumu ya nchi wanachama wa mkataba**

- **Kuandaa na Kutekeleza Programu za Kitaifa za Kupambana na Kuenea kwa Jangwa:** Nchi wanachama zinawajibika kuandaa na kutekeleza Programu za Kitaifa za Kupambana na Kuenea kwa Jangwa (National Action Programmes – NAPs) kwa kushirikisha wadau mbalimbali, ili kukabiliana na uharibifu wa ardhi na ukame kwa njia endelevu.

- **Kuzuia na Kupunguza Uharibifu wa Ardhi:** Nchi zinapaswa kuchukua hatua za kuzuia, kupunguza na kurejesha ardhi iliyoharibika kupitia usimamizi endelevu wa ardhi, kilimo hifadhi, uhifadhi wa maji na urejeshaji wa mifumo ya ikolojia.

- **Kukabiliana na Athari za Ukame:** Nchi wanachama zinatakiwa kuandaa mikakati ya kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na athari za ukame, ikiwemo mifumo ya tahadhari ya mapema, usimamizi wa rasilimali za maji na hatua za kupunguza athari kwa jamii zilizo hatarini

- **Kushirikisha Jamii na Wadau Wengine:** Nchi zinawajibika kuhakikisha ushiriki wa jamii za maeneo yaliyoathirika, sekta binafsi, asasi za kiraia na wadau wengine katika upangaji na utekelezaji wa hatua za kupambana na kuenea kwa jangwa.

- **Kukuza Utafiti, Elimu na Kujenga Uwezo:** Nchi wanachama zinahimizwa kuendeleza utafiti wa kisayansi, ukusanyaji wa takwimu, elimu na mafunzo ili kuongeza uelewa na uwezo wa kitaifa katika kukabiliana na uharibifu wa ardhi na ukame.

- **Kuingiza Masuala ya Uharibifu wa Ardhi katika Mipango ya Maendeleo:** Nchi zinapaswa kuzingatia masuala ya uharibifu wa ardhi, ukame na usimamizi endelevu wa ardhi katika sera, mipango na bajeti za maendeleo ya kitaifa na sekta mbalimbali.

- **Kutoa Taarifa na Kushirikishana Uzoefu:** Nchi wanachama zina wajibu wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mkataba kwa Sekretarieti ya UNCCD, pamoja na kushirikishana uzoefu, mbinu bora na taarifa kati ya nchi wanachama

- **Kukuza Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa:** Nchi zinapaswa kushirikiana kikanda na kimataifa katika utekelezaji wa mkataba, hususan katika maeneo yanayoshirikiana ikolojia kama vile maeneo kame, nusu kame na maeneo yanayokumbwa na ukame.

- **Kutafuta na Kusimamia Rasilimali za Kifedha:** Nchi wanachama zinatakiwa kuhamasisha na kusimamia rasilimali za kifedha kutoka ndani na nje ya nchi, ikiwemo mifuko ya kimataifa kama Global Environment Facility (GEF), kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UNCCD.

## 5. Shughuli/miradi inayotekelezwa chini ya mkataba

Kwa kuwa utekelezaji wa shughuli chini ya Mkataba ni Mtambuka, Wadau mbalimbali wamekuwa wakitekeleza miradi ambayo inalenga kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Miradi hii inatekelezwa katika Sekta za Maji, Misitu, Kilimo, Ardhi, Mifugo na Wanyamapori. Utekelezaji huu pia unashirikisha Asasi zisizo za Kiaserikali; Washiriki wa Maendeleo, Asasi za Kidini; Sekta binafsi na Jamii kwa ujumla. Miradi kama SLR, EBARR, LDFS, Miumbo, Uhifadhi wa Bonde la Ziwa Nyasa, Viktoria na Tanganyika ni sehemu kubwa ya Miradi inayotekeleza shughuli chini ya Mkataba huu.

## 6. Faida za mkataba

- Upatikanaji wa rasilimali za kifedha za kimataifa
- Msaada wa kiufundi na kitaalamu
- Kujenga uwezo wa kitaifa
- Ushirikiano wa kikanda na kimataifa
- Kubadilishana uzoefu na mbinu bora

## 7. Mafanikio ya utekelezaji wa mkataba

Yapo mafanikio kadha wa kadha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwanachama wa Mktataba huu. Mafanikio haya ni pamoja na ushiriki wa Mikutano, upatikanaji wa miradi, upatikanaji wa fedha kupitia mifuko ya kimazingira kama GEF, AF, LDCF, GCF na mingine katika kaliba ya Mazingira. Mafanikio mengine ni kuongeza ushirikiano na wadau kama vile Sekta za Serikali, Taasisi za Umma; Washirka wa Maendeleo; Asasi za Kirai; Sekta binafsi; Taasisi za kidini; na Jamii kwa ujumla.

## 8. Changamoto zinazokabili utekelezaji wa mkataba

- Ushiriki hafifu wa Sekta katika masuala ya kupambana na kuenea kwa Jangwa
- Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya kupambana na kuenea kwa Jangwa
- Changamoto ya mafungu ya utekelezaji wa shughuli chini ya Mkataba; na
- Changamoto ya uratibu wa shughuli chini ya Mkataba hasa Sekretarieti ya Mkataba.